HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI
MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE 23/10/2021 KATIKA OFISI YA MCHUMI WA MANISPAA.

WAJUMBE WALIOHUDHURIA

1. Monica Sana - Mwenyekiti
2. Edward Mushi - Katibu
3. Richard Sanga - Mjumbe
4. Rose Y. Minja - Mjumbe
5. Masalu Bunani - Mjumbe
6. Linda Samu - Mjumbe
7. Adv. Leah Francis - Mwanasheria wa Manispaa – Mwalikwa

SEKRETARIETI

1. Dominian Mpombe - Afisa Manunuzi

MUHT NA. 01/10/2021: KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti alifungua kikao saa 12:00 Mchana na kuwakaribisha wajumbe wote katika kikao.

MUHT NA. 02/10/2021: KUTHIBITISHA AJENDA

Ajenda zifuatazo zilithibitishwa kuwa ajenda sahihi za kikao hicho.

1. Kufungua Kikao.
2. Kuthibitisha agenda
3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha tarehe **14/06/2021**
4. Yatokanayo na kikao cha tarehe **14/06/2021**
5. Kupitia ripoti ya Timu ya Tathimini zabuni ya ***"Construction of 22 Classrooms for Secondary Schools at Moshi Municipal Council"***
   Zabuni Na: LGA/045/2021-2022/HQ/W/93
6. Mengineyo
7. Kufunga Kikao

MUHT NA. 03/10/2021: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA TAREHE 14/06/2021

Muhtasari huo ulisomwa na kisha Mwenyekiti na Katibu wakaweka saini kuwa kumbukumbu sahihi za kikao hicho.

MUHT NA. 04/10/2021: YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 14/06/2021

Hakukuwa na yatokanayo katika kikao hicho

MUHT NA. 05/10/2021: KUPITA RIPOTI YA TIMU YA TATHIMINI ZABUNI YA "CONSTRUCTION OF 22 CLASSROOMS FOR SECONDARY SCHOOLS AT MOSHI MUNICIPAL COUNCI".

Halmashauri ya Manispaa ya Moshi ilitangaza zabuni husika mnamo tarehe **19/10/2021** na kufunguliwa tarehe **22/10/2021** ambapo wazabuni wawili waliomba kazi hiyo kama ifuatavyo:-

NA	JINA LA MZABUNI	KIASI
1	M/s. J.S. KHAMBHAITA LTD, S.L.P. 65, **MOSHI**	605,916,000/= VAT INCLUSIVE
2	M/s. RAVJI CONSTRUCTION LTD, S.L.P. 8322 **MOSHI**	439,843,000/= VAT INCLUSIVE

Timu ya Tathimini ilimpendekeza Mkandarasi M/s. Ravji Construction Ltd, apewe kazi hiyo kwa gharama ya Shs. **439,843,000/= VAT INCLUSIVE.**

MAPENDEKEZO YA PMU:

PMU imeridhia mapendekezo ya Timu ya Tathimini kuwa Mkandarasi **M/s. Ravji Construction Ltd,** apewe kazi hiyo kwa gharama ya Shs. **439,843,000/= VAT INCLUSIVE.**

MAAMUZI YA BODI YA ZABUNI:

Bodi ya Zabuni imeridhia mapendekezo ya PMU Mkandarasi huyo apewe kazi hiyo na asimamiwe na Kamati atakayounda Mkurugenzi kuhakikisha ujenzi wa madarasa na samani zake unakamilika kabla ya tarehe 15/12/2021.

MUHT NA. 06/10/2021:

Hakukuwa na mengineyo katika kikao hicho

MUHT NA. 07/10/2021: KUFUNGA KIKAO

Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 7:30 Mchana

UMETHIBITISHWA

....

MWENYEKITI **KATIBU**

TAREHE ...12/11/2021.....